# SHERIA YA KUANZISHA JUMUIYA YA MAWAKILI ZANZIBAR, KUWEKA MALENGO, UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA JUMUIYA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza Kutumika.

2. Ufafanuzi.

### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA JUMUIYA YA MAWAKILI

3. Kuanzishwa kwa Jumuiya.

4. Malengo na Kazi za Jumuiya.

5. Uwezo wa jumla wa Jumuiya.

6. Misingi ya uongozaji.

7. Jumuiya haitafungamana na mrengo wa kisiasa.

### SEHEMU YA TATU
### UANACHAMA WA JUMUIYA

8. Uanachama.

9. Wanachama wa heshima.

10. Haki na fursa kwa wanachama.

11. Kusimamishwa, kufukuzwa au kuzuiliwa.

12. Kusita kwa mwanachama.

13. Ada ya mwaka ya Jumuiya.

## SEHEMU YA NNE
## VYOMBO VYA JUMUIYA

14. Vyombo vya Jumuiya.

15. Mkutano Mkuu.

16. Kazi za Mkutano Mkuu.

17. Uwezo wa Mkutano Mkuu.

18. Mkutano wa Dharura.

19. Akidi.

20. Baraza la Jumuiya.

21. Kazi za Baraza.

22. Uwezo wa Baraza.

23. Kusita kuwa mjumbe wa Baraza.

24. Mkutano wa Baraza.

25. Mkutano maalumu wa Baraza.

26. Kuitisha na utaratibu wa mikutano ya Baraza.

27. Maazimio ya Baraza.

28. Utaratibu wa upigaji kura.

29. Marekebisho ya azimio.

30. Kuhifadhiwa kwa Kumbukumbu.

31. Sekretarieti.

32. Muundo wa sekretarieti.

33. Afisa Mtendaji Mkuu.

## SEHEMU YA TANO
## FEDHA NA MATUMIZI YA JUMUIYA

34. Vyanzo vya mapato vya Jumuiya.

35. Matumizi ya Fedha.

36. Uwekaji wa hesabu.

37. Taarifa na hesabu.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

38. Nafasi ya Mwanasheria Mkuu kwa Jumuiya.

39. Uchaguzi.

40. Adhabu ya Jumla.

41. Kanuni ndogo.

42. Kanuni.

43. Kufutwa kwa Usajili na Kubakiza.

**SHERIA NAMBA 7 YA 2019**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

21 Oktoba, **2019**

# SHERIA YA KUANZISHA JUMUIYA YA MAWAKILI ZANZIBAR, KUWEKA MALENGO, UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA JUMUIYA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza Kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Jumuiya ya Mawakili Zanzibar, 2019 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Wakili" maana yake ni mtu aliyesajiliwa na kukubaliwa kuwa wakili wa kujitegemea chini ya masharti ya sheria husika;

"Mwanasheria Mkuu" maana yake ni Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar aliyeteuliwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Jaji Mkuu" maana yake ni Jaji Mkuu wa Zanzibar aliyeteuliwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Jumuiya ya Mawakili Zanzibar lililoanzishwa chini ya kifungu cha 20 cha Sheria hii;

"Mkurugenzi wa Mashtaka" maana yake ni Mkurugenzi wa Mashtaka aliyeteuliwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Mwanasheria wa kigeni" maana yake ni mtu ambaye ameruhusiwa au kusajiliwa kufanya kazi ya uwakili katika nchi yoyote isiyokuwa Zanzibar kwa mamlaka ya kigeni ambayo imepewa kazi kwa mujibu wa sheria ya uidhinishaji au usajili wa mtu kufanya kazi ya uwakili katika nchi hiyo;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Mthibitishaji rasmi" maana yake ni wakili aliyefanya kazi za uwakili ambaye ameruhusiwa kuwa mthibitishaji rasmi na Jaji Mkuu;

"Viongozi wa Ofisi" maana yake ni Rais wa Jumuiya, Makamu wa Rais na Mweka Hazina;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Rais wa Jumuiya" maana yake ni Rais wa Jumuiya ya Mawakili Zanzibar aliyechaguliwa chini ya kifungu cha 39 cha Sheria hii;

"Jumuiya" maana yake ni Jumuiya ya Mawakili Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA JUMUIYA YA MAWAKILI

Kuanzishwa kwa Jumuiya.

**3.** Kunaanzishwa chombo kinachojitegemea kitakachojulikana kama Jumuiya ya Mawakili Zanzibar ambacho ni endelevu na chenye muhuri wake, na kwa jina lake kina uwezo wa:

(a) kushtaki au kushtakiwa;

(b) kuingia katika mikataba;

(c) kuchukua, kununua au vyenginevyo kujipatia, kuzuia, kuendeleza au kuondosha mali inayohamishika au isiyohamishika;

(d) kukopa au kuchangisha fedha;

(e) kuwekeza na kutunza fedha za Jumuiya ambazo hazihitajiki kwa haraka kwa namna ambayo inaweza kuamuliwa na Jumuiya kila baada ya muda; na

(f) kufanya au kutekeleza mambo mengine yoyote au vitendo ambavyo kisheria vinaweza kufanywa na chombo kinachojitegemea.

Malengo na Kazi za Jumuiya.

**4.**-(1) Jumuiya itakuwa na malengo yafuatayo:

(a) kuilinda Katiba ya Zanzibar na kukuza utawala wa sheria na usimamizi wa haki;

(b) kuhakikisha kwamba mawakili wote ambao wanafanya kazi ya uwakili au wanatoa huduma za uwakili wanakidhi viwango vya mafunzo, uwezo wa kitaaluma na maadili ya kitaaluma ambayo ni sahihi kwa huduma za uwakili wanazozitoa;

(c) kuwezesha upatikanaji wa taaluma ya sheria kwa wanachama wa Jumuiya na watoaji wa huduma wasaidizi, ikijumuisha wasaidizi wa sheria kupitia ukuzaji wa viwango vya juu vya elimu na mafunzo ya sheria;

(d) kuwezesha utambuzi wa mageuzi ya mfumo wa taaluma ya sheria ambao utakuwa imara, wa uwajibikaji, wa ufanisi na unaojitegemea;

(e) kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya utoaji wa fursa sawa kwa mawakili wote Zanzibar;

(f) kulinda na kukuza maslahi ya watumiaji wa huduma za sheria na maslahi ya wananchi kwa ujumla, kwa kutoa haki, ubora, ufanisi na kwa utaratibu wa wazi kwa ajili ya maamuzi ya malalamiko dhidi ya mawakili; na

(g) kuwashajihisha mawakili wa Zanzibar kufanya kazi nje ya Zanzibar.

(2) Jumuiya itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuwasaidia wananchi wa Zanzibar katika masuala yanayohusiana na sheria;

(b) kuweka, kudumisha na kuendeleza viwango vya mafunzo, uwezo wa kitaalamu na maadili ya kitaalamu kwa utoaji wa huduma za kisheria Zanzibar;

(c) kuweka, kuendeleza na kukuza viwango vya utendaji kitaaluma, maadili ya kiutendaji, na mafunzo kwa ajili ya taaluma ya sheria Zanzibar;

(d) kuwakilisha, kulinda na kuwasaidia wanachama wa taaluma ya sheria Zanzibar katika mambo yanayohusiana na masharti ya utendaji na maslahi;

(e) kuendeleza na kuwezesha mipango ya mafunzo stahiki kwa mawakili; na

(f) kufanya mambo yote mengine yanayohusiana au yanayoendana na kazi zake.

Uwezo wa jumla wa Jumuiya.

**5.** Jumuiya itakuwa na uwezo wa kufanya mambo yote muhimu kwa ajili ya upatikanaji wa mafanikio stahiki ya malengo ya Jumuiya na utekelezaji wa kazi zake.

Misingi ya uongozaji.

**6.** Katika kutekeleza kazi na uwezo wake chini ya Sheria hii, Jumuiya itazingatia misingi ifuatayo:

(a) uendelezaji wa amani, umoja na mshikamano;

(b) uhifadhi na uendelezaji wa masuala ya kikatiba, haki na utawala wa sheria;

(c) uwezeshaji wa upatikanaji wa haki;

(d) ulinzi wa maslahi ya umma; na

(e) uhifadhi wa heshima na taaluma.

Jumuiya haitafungamana na mrengo wa kisiasa.

**7.** Jumuiya itakuwa ni chombo cha kitaalamu na kwa madhumuni hayo haitokuwa na mrengo wa kisiasa na haitajiingiza, haitajihusisha au kufungamana na mambo yoyote ya kisiasa ya chama chochote cha siasa au mambo ya uchaguzi wa kisiasa.

## SEHEMU YA TATU
## UANACHAMA WA JUMUIYA

Uanachama.

**8.** Jumuiya itaundwa na:

(a) wanasheria wote na wathibitishaji rasmi waliosajiliwa na sheria husika;

(b) watu wote waliosajiliwa na waliokubalika chini ya Sheria hii; na

(c) watu wote waliotajwa kama wanachama wa heshima wa Jumuiya kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Sheria hii.

Wanachama wa heshima.

**9.**-(1) Baraza linaweza kuteua watu mashuhuri katika fani ya sheria kuwa wanachama wa heshima wa kudumu au kwa kipindi ambacho Baraza litaona inafaa.

(2) Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka au Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar baada ya kustaafu anaweza kuwa mwanachama wa kudumu wa heshima wa Jumuiya.

(3) Mwanachama wa heshima hatotakiwa kulipa ada yoyote au michango mengine yoyote itakayotozwa kwa wanachama kila baada ya muda.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Baraza kabla ya kuteua watu mashuhuri, litazingatia sifa, ujuzi, taaluma na uzoefu wa wahusika.

Haki na fursa kwa wanachama.

**10.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, wanachama wa Jumuiya watakuwa na haki na fursa sawa.

(2) Wanachama hai watastahiki kupiga kura katika mikutano mikuu ya Jumuiya.

(3) Mtu, asiyekuwa mwanachama hai, ambaye ni mkaazi chini ya sheria za Zanzibar, hatokuwa na sifa ya kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza.

Kusimamishwa, kufukuzwa au kuzuiliwa.

**11.**-(1) Kwa madhumuni ya masharti ya Sheria hii, Baraza linaweza kumsimamisha, kumfukuza au kumzuilia sehemu au haki zote au fursa mwanachama yeyote asiyekuwa mwanachama wa heshima kwa namna na sababu zilizoelezwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Mwanachana hatosimamishwa, hatofukuzwa au kuzuiliwa sehemu au haki au fursa zote isipokuwa atapewa fursa ya kujibu tuhuma zote zilizotolewa dhidi ya mwanachama huyo.

(3) Mwanachama ambaye amesimamishwa au kufukuzwa katika Jumuiya hatostahiki, katika kipindi ambacho amesimamishwa au kufukuzwa, kupatiwa haki au fursa yoyote ya uwanachama.

(4) Mwanachama wa Jumuiya ambae atakuwa amesimamishwa au kufukuzwa katika Jumuiya, chombo kilichompa ruhusa ya kufanya kazi za uwakili kitafuta au kusimamisha ruhusa hiyo.

Kusita kwa uanachama.

**12.** Mwanachama wa Jumuiya, asiyekuwa mwanachama wa heshima, ambaye ana cheti cha kufanya kazi za uwakili ataendelea kuwa mwanachama hadi:

(a) mwisho wa mwaka ambao cheti hicho kimetolewa; au

(b) pale jina lake limeondolewa kutoka katika Daftari la Mawakili.

Ada ya mwaka ya Jumuiya.

**13.**-(1) Kiwango cha ada ya mwaka kwa wanachama wa Jumuiya kinachostahiki kulipwa chini ya Sheria hii, kitapangwa na Baraza kila baada ya muda kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki.

(2) Ada ya mwaka italipwa na wanachama kila mwaka kabla ya Mkutano Mkuu wa Jumuiya.

(3) Katika kupanga kiwango cha ada ya mwaka, Baraza litakuwa huru kuzigawa ada hizo katika madaraja tofauti ambayo yanaweza kulipwa na makundi ya wanachama kama Baraza litakavyoona inafaa.

(4) Baraza linaweza, kila baada ya muda kwa madhumuni ya Jumuiya, kupanga tozo nyengine zitakazolipwa na wanachama wote wanaowajibika kulipa ada ya mwaka chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA NNE
## VYOMBO VYA JUMUIYA

Vyombo vya Jumuiya

**14.** Kwa uendeshaji mzuri wa Jumuiya kutakuwa na vyombo vya Jumuiya vifuatavyo:

(a) Mkutano Mkuu;

(b) Baraza; na

(c) Sekretarieti.

Mkutano Mkuu.

**15.**-(1) Mkutano Mkuu utakuwa ndio chombo cha juu cha Jumuiya.

(2) Jumuiya itafanya Mkutano Mkuu mmoja ndani ya miezi sita baada ya tarehe 31 Disemba ya kila mwaka katika mahali kama itakavyoamuliwa na Baraza.

(3) Mkutano Mkuu utajumuisha wanachama wote wa Jumuiya.

(4) Afisa Mtendaji Mkuu atakuwa Katibu wa Mkutano Mkuu wa Jumuiya.

(5) Gharama za Mkutano Mkuu zitatokana na fedha za Jumuiya.

(6) Taarifa ya Mkutano Mkuu itatolewa na Baraza angalau siku thelathini kabla ya tarehe ya Mkutano.

(7) Rais wa Jumuiya ataongoza Mkutano Mkuu na akiwa hayupo Makamu wa Rais ataongoza Mkutano Mkuu.

(8) Mkutano Mkuu unaweza kujipangia utaratibu wake, na hususani katika uitishaji wa mikutano, taarifa itakayotolewa ya mikutano, uendeshaji mikutano, uwekaji wa kumbukumbu, uhifadhi, utoaji na uchunguzi wa kumbukumbu hizo.

Kazi za Mkutano Mkuu.

**16.** Mkutano Mkuu utakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuandaa sera za msingi za Jumuiya;

(b) kupokea na kuthibitisha taarifa za utendaji za Jumuiya;

(c) kuidhinisha maazimio na maamuzi yote ya Jumuiya;

(d) kupitia na kuidhinisha bajeti ya mwaka ya Jumuiya; na

(e) kusimamia kwa ujumla kazi za Jumuiya.

Uwezo wa Mkutano Mkuu.

**17.** Mkutano Mkuu utakuwa na uwezo ufuatao:

(a) kuchagua viongozi wa ofisi;

(b) kuchagua wajumbe wengine watano wa Baraza kwa kuzingatia jinsia;

(c) kumsimamisha mwanchama wa Jumuiya;

(d) kutekeleza uwezo mwengine wowote uliotolewa chini ya Sheria hii; na

(e) kumfukuza mwanachama ikibainika amevuja taratibu za Jumuiya.

Mkutano wa Dharura.

**18.**-(1) Mkutano mwengine wowote wa Jumuiya usiokuwa Mkutano Mkuu utajulikana kama ni Mkutano wa Dharura na unaweza kuitishwa muda wowote endapo Baraza litaona inafaa.

(2) Mkutano Mkuu unaweza kuombwa kufanyika na thuluthi mbili ya wanachama hai kwa kutoa taarifa ya maandishi iliyosainiwa na wanachama wote hao kwa kuainisha ajenda ya mkutano unaopendekezwa.

(3) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, taarifa itapelekwa kwa Afisa Mtendaji Mkuu.

(4) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu cha 15 cha Sheria hii, taarifa fupi isiyozidi siku thelathini inaweza kutolewa wakati ambao Baraza litaona inafaa.

(5) Masharti ya kifungu cha 15 cha Sheria hii yatatumika sawa katika Mikutano ya Dharura.

Akidi.

**19.**-(1) Akidi ya Mkutano Mkuu itakuwa angalau zaidi ya nusu ya wanachama hai wote wa Jumuiya.

(2) Masuala yote yatakayojitokeza katika mikutano yataamuliwa kwa maafikiano.

(3) Endapo maamuzi hayakufikiwa kwa maafikiano chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, masuala yataamuliwa kwa wingi wa kura za wanachama waliohudhuria.

(4) Mwenyekiti katika Mkutano Mkuu atakuwa na kura ya ujumbe na endapo kura zitakuwa sawa, atakuwa na kura ya maamuzi.

Baraza la Jumuiya.

**20.**-(1) Kutakuwa na Baraza ambalo litakuwa ni chombo cha uendeshaji cha Jumuiya.

(2) Baraza litaundwa na:

(a) Viongozi wa Ofisi; na

(b) Wajumbe wengine watano watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu angalau wawili miongoni mwao wawe wanawake.

(3) Afisa Mtendaji Mkuu atakuwa Katibu wa Baraza.

Kazi za Baraza.

**21.**-(1) Baraza litakuwa na kazi za jumla za kusimamia na kudhibiti mambo ya Jumuiya.

(2) Bila ya kuathiri kazi za jumla chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Baraza litakuwa na kazi maalumu za:

(a) kujibu masuala yanayoathiri utendaji kazi na miiko ya taaluma, mwenendo na nidhamu ya wanachama wake;

(b) kutambuwa jambo lolote linaloathiri Jumuiya au mwenendo wa taaluma ya wanachama wake;

(c) kuwasilisha mbele ya Mkutano Mkuu wa Jumuiya jambo lolote ambalo inaloliona ni muhimu kwa Jumuiya au kwa maslahi ya taaluma na kutoa mapendekezo yoyote na kuchukuwa hatua kama itakavyoona inafaa kuhusiana na jambo hilo;

(d) kuwawakilisha wanachama wa Jumuiya au sehemu ya wanachama katika jambo lolote ambalo linaweza kuwa la muhimu au haraka;

(e) kununua, kukodi au vyenginevyo kujipatia na kutafuta maeneo yanayofaa kwa ajili ya matumizi ya Jumuiya;

(f) kuwasiliana, kila baada ya muda na vyombo vyengine vinavyofanana na wanachama wa taaluma katika maeneo mengine kwa ajili ya kupata na kubadilishana taarifa juu ya mambo yote yatakayoleta faida au maslahi kwa wanachama;

(g) kupeleka malalamiko au madai yaliyofanywa na au dhidi ya Jumuiya kwa ajili ya upatanishi na kwa kuzingatia na kutekeleza kila uamuzi uliofanywa kutokana na usuluhishi na kupendekeza wasuluhishi ikiwa itaombwa kufanya hivyo;

(h) kufanya na kutoa stakabadhi, malipo mengine ya fedha yanayolipwa kwa malalamiko na au kwa madai ya Jumuiya;

(i) kuunda au kushiriki katika uundaji wa kampuni yoyote kwa madhumuni ya utekelezaji wa kazi zote au sehemu ya kazi za Jumuiya;

(j) kukopa au kuchangisha fedha kutokana na deni la benki au vyenginevyo kwa kuweka rehani au dhamana nyengine zitakazokuwepo au zitakazohusu mali zote au sehemu na haki za Jumuiya au bila dhamana yoyote hiyo na kwa kuzingatia vigezo vya vipaumbele au vyenginevyo kama Baraza litakavyoona inafaa; na

(k) kutekeleza kazi nyengine yoyote ambayo haijaelezwa katika Sheria hii na inatakiwa kutekelezwa na wanachama wa Jumuiya katika Mkutano Mkuu.

(3) Katika utekelezaji kazi zake chini ya Sheria hii, Baraza litahakikisha kwamba Jumuiya haitumiki kwa madhumuni yoyote yatakayopelekea utabaka, udini, ubaguzi au namna nyengine yoyote ya tendo ambalo halitoi taswira nzuri ya Jumuiya.

Uwezo wa Baraza.

**22.** Baraza litakuwa na uwezo wa:

(a) kutunga Kanuni ndogo kwa mambo yote ambayo hayajaelezwa kuwa ni ya Jumuiya katika Mkutano Mkuu ikiwa yameelezwa kuwa ni miongoni mwa uwezo wake au hayajaelezwa;

(b) kuteua kupitia mamlaka yake maofisa, makarani, mawakala na watumishi wa kudumu, wa muda au kwa huduma maalum kama litakavyoona inafaa kila baada ya muda na kuainisha majukumu yao na masharti ya huduma;

(c) kufungua, kutetea, au kufanya mazungumzo ya malipo juu ya shauri lolote lililofunguliwa na au dhidi ya Jumuiya au maofisa wake au vyenginevyo linalohusu masuala ya Jumuiya na kufanya mazungumzo ya malipo na kuruhusu muda wa malipo hayo au kuridhia madeni yoyote yaliyopo au malalamiko yoyote au madai yaliyofanywa na au dhidi ya Jumuiya; na

(d) kutekeleza uwezo mwengine wowote ambao haujaelezwa katika Sheria hii, na unatakiwa kutekelezwa na wanachama wa Jumuiya katika Mkutano Mkuu.

Kusita kuwa mjumbe wa Baraza.

**23.** Mjumbe wa Baraza atasita kushika madaraka ikiwa:

(a) amesita kuwa mwanachama wa Jumuiya;

(b) amejiuzulu;

(c) amefariki;

(d) amesita kuwa mjumbe wa Baraza kwa maazimio ya idadi kubwa ya wanachama katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya;

(e) amefutwa katika Daftari la Mawakili au amesimamishwa kufanya kazi za uwakili au ametiwa hatiani kwa kosa linalohusisha udanganyifu au kukosa uaminifu;

(f) ametangazwa na mamlaka yenye uwezo kuwa hana akili timamu au ana ugonjwa wa kimwili ambao unamfanya ashindwe kutekeleza majukumu yake;

(g) ametangazwa na mahakama yenye uwezo kuwa amefilisika; au

(h) ameshindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya kulitaarifu Baraza.

Mkutano wa Baraza.

**24.**-(1) Baraza litakutana angalau mara moja katika kila miezi mitatu na linaweza kukutana wakati wowote inapohitajika.

(2) Akidi ya kikao cha Baraza itakuwa angalau nusu ya wajumbe wote.

Mkutano maalumu wa Baraza.

**25.** (1) Mkutano maalumu wa Baraza utaitishwa muda wowote ikiwa utatakiwa kufanyika na angalau nusu ya wajumbe wote wa Baraza.

(2) Baraza litaitisha mkutano maalumu wa Baraza ndani ya siku kumi nne baada ya kupokea maombi yaliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Kuitisha na utaratibu wa mikutano ya Baraza.

**26.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, namna ya kuitisha mikutano ya kawaida au mikutano maalumu ya Baraza na utaratibu wa mikutano hiyo, itakuwa kama Baraza litakavyoweza kuainisha kila baada ya muda.

Azimio la Baraza.

**27.**-(1) Azimio la Baraza katika Mkutano litapitishwa kwa maafikiano.

(2) Endapo maafikiano chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hayakufikiwa, azimio litapitishwa kwa wingi wa kura za wajumbe wa Baraza waliohudhuria.

(3) Mwenyekiti katika mkutano wa Baraza atakuwa na kura ya ujumbe na endapo ikitokezea usawa wa kura atakuwa na kura ya maamuzi.

Utaratibu wa upigaji kura.

**28.** Utaratibu wa upigaji wa kura katika mikutano utakuwa kama itakavyoainishwa na Kanuni ndogo zitakazotungwa na Baraza chini ya Sheria hii.

Marekebisho ya azimio.

**29.**-(1) Azimio la Baraza katika mkutano halitorekebishwa au kubatilishwa isipokuwa kwa azimio maalumu la Baraza litakalopitishwa dhidi ya azimio hilo la awali.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "azimio maalumu" maana yake ni azimio lililopitishwa na wajumbe wasiopungua theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza waliohudhuria na kupiga kura katika mkutano wa Baraza ulioitishwa kwa nia ya kupendekeza azimio hilo.

Kuhifadhiwa kwa Kumbukumbu.

**30.** Baraza litawezesha kuchukuliwa na kuhifadhiwa kumbukumbu sahihi za mikutano yote ya Baraza.

Sekretarieti.

**31.**-(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Jumuiya ambayo itaongozwa na Afisa Mtendaji Mkuu.

(2) Sekretarieti itakuwa na jukumu la kusimamia masuala ya Jumuiya ya kila siku.

(3) Sekretarieti, kila baada ya muda, itapokea maelekezo ya jumla au maalumu kutoka kwenye Baraza kupitia Afisa Mtendaji Mkuu.

Muundo wa sekretarieti.

**32.**-(1) Sekretarieti itaundwa kwa namna ya kukuza uwajibikaji kwa utendaji ulio na ufanisi na kumjali mteja katika taaluma.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Sekretarieti itaundwa na idara zifuatazo:

(a) Idara ya viwango vya utendaji kazi za uwakili ambayo itakuwa na wajibu wa kukuza utendaji ulio na ufanisi; kumjali mteja na kufanikisha kufuata kwa ukamilifu kanuni za utendaji katika taaluma kupitia ushauri, kusaidia na aina nyengine ya misaada kwa mawakili na kampuni za kisheria;

(b) Idara ya utekelezaji na maadili ambayo itakuwa na wajibu wa kupokea na kutathimini malalamiko dhidi ya mawakili na uwendeshaji wa kesi mbele ya Kamati ya Maadili;

(c) Idara ya maendeleo ya taaluma endelevu ambayo itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa wanachama wanafuata kanuni husika; na

(d) Idara nyengine yoyote ambayo Baraza linaweza, kila baada ya muda, kuanzisha endapo litaona inafaa.

Afisa Mtendaji Mkuu.

**33.**-(1) Kutakuwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ambaye atakuwa dhamana wa Sekretarieti ya Jumuiya.

(2) Afisa Mtendaji Mkuu atateuliwa na Baraza kwa utaratibu wa uajiri ulio wa uwazi na ushindani.

(3) Afisa Mtendaji Mkuu atawajibika kwa Baraza kwa usimamizi na uendeshaji wa kila siku wa Sekretarieti, masuala na kazi za Jumuiya kama Baraza litakavyoamua.

(4) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika utawala wa umma, sheria au fani nyengine zinazolingana na hizo;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka mitano; na

(d) ni mwaminifu na mwenye tabia njema.

(5) Mtu aliyeteuliwa kuwa Afisa Mtendaji Mkuu atashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuwa na sifa ya kuteuliwa tena baada ya kuidhinishwa na Baraza.

(6) Afisa Mtendaji Mkuu anaweza kuondolewa madarakani na Baraza kwa kuwepo sababu za msingi na kwa utaratibu utakaoelezwa katika Kanuni ndogo.

## SEHEMU YA TANO
## FEDHA NA MATUMIZI YA JUMUIYA

Vyanzo vya fedha vya Jumuiya.

**34.**-(1) Vyanzo vya fedha vya Jumuiya vitatokana na:

(a) ada zozote za mwaka zitakazolipwa kwa Jumuiya;

(b) riba zote, faida na mapato mengine au faida inayotokana na uwekezaji wa fedha za Jumuiya;

(c) mapato yanayotokana na uwekezaji wowote wa fedha za Jumuiya;

(d) fedha zote zilizokopwa kwa madhumuni ya Jumuiya;

(e) fedha nyengine zozote ambazo zinazoweza kumilikiwa au zinazotokana na Jumuiya au zimepokelewa na Baraza kwa ajili ya Jumuiya.

Matumizi ya fedha.

**35.**-(1) Fedha za Jumuiya zitatumika kwa:

(a) gharama ilizoingia Jumuiya katika kutekeleza kazi zake na mikutano chini ya Sheria hii;

(b) uwekezaji wa fedha ambazo ni sehemu ya fedha za Jumuiya na hazihitajiki wakati huo kwa matumizi mengine yoyote;

(c) kurejesha fedha zote zilizokopwa na Jumuiya na malipo ya riba kwa fedha zilizokopwa; na

(d) kulipa fidia au kupunguza hasara endapo imethibitika na kuridhiwa na Baraza kwamba mtu yeyote amepata hasara kutokana na udanganyifu wa wakili kuhusiana na utendaji kazi wa uwakili Zanzibar.

(2) Malipo chini ya aya (d) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hayatafanywa kuhusiana na hasara yoyote isipokuwa taarifa ya hasara hiyo imepokelewa na Jumuiya kwa namna na ndani ya wakati baada ya hasara hiyo kujulikana na mtu ambaye alipata hasara hiyo kama itakavyoweza kuainishwa na Kanuni ndogo.

(3) Baraza linaweza kutunga Kanuni ndogo kuhusiana na utaratibu wa kufuatwa kwa ajili ya kutekeleza kifungu hiki na kuhusiana na jambo lolote litakalojitokeza, litakalochangia kwa masharti haya au linalohusiana na uendeshaji au uhifadhi wa fedha.

Uwekaji wa hesabu.

**36.**-(1) Baraza litasababisha kuwekwa na kukaguliwa hesabu za fedha zote, mali na rasilimali za Jumuiya tarehe 31 Disemba ya kila mwaka na mkaguzi atakayeteuliwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa Jumuiya.

(2) Mkaguzi atakayeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hatokuwa mwanachama wa Jumuiya.

Taarifa na hesabu.

**37.** Kwa kadri itakavyowezekana baada ya tarehe 31 Disemba ya kila mwaka, Baraza litawasilisha kwa Jumuiya katika Mkutano Mkuu taarifa kamili ya shughuli za Jumuiya ikijumuisha shughuli za Baraza na za kamati yoyote iliyoteuliwa na Baraza, pamoja na hesabu zilizokaguliwa kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria hii, kwa miezi kumi na mbili ya mwaka uliomalizika.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

Nafasi ya Mwanasheria Mkuu kwa Jumuiya.

**38.**-(1) Mwanasheria Mkuu kama Mkuu wa Mawakili atafanya kazi kwa kushirikiana na Jumuiya katika masuala yanayohusiana na utendaji kazi za uwakili Zanzibar na atahakikisha Jumuiya inatekeleza kazi zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Endapo itatokea kwa maoni ya Mwanasheria Mkuu kwamba, Jumuiya inatekeleza kazi zake kinyume na masharti na malengo ya Sheria hii, Mwanasheria Mkuu ataliita Baraza kulizungumzia jambo hilo.

Uchaguzi.

**39.**-(1) Kutakuwa na uchaguzi wa Jumuiya wa kuchagua Viongozi wa Ofisi na wajumbe wa Baraza.

(2) Wanachama wote wa Jumuiya wenye sifa ya kupiga kura chini ya Sheria hii, watashiriki kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka kwa uchaguzi wa Rais wa Jumuiya, Makamu wa Rais wa Jumuiya, Mweka hazina na wajumbe watano wa Baraza.

(3) Mpiga kura yeyote mwenye sifa chini ya Sheria hii ambaye atashawishika kuwa mgombea katika uchaguzi huo, atapeleka maombi kwa Baraza siku kumi na nne kabla ya uchaguzi.

(4) Watumishi wa umma, mtu yeyote mwenye nafasi ya uongozi katika chama cha kisiasa, wabunge, wawakilishi pamoja na madiwani hawaruhusiwi kugombea katika nafasi yoyote ya uongozi chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki;

(5) Rais wa Jumuiya atakuwa ni Mzanzibari ambaye ataongoza mikutano yote ya Jumuiya na Baraza.

(6) Wajumbe watakaochaguliwa chini ya kifungu hiki watashika madaraka kwa kipindi cha mwaka mmoja na wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Adhabu ya jumla.

**40.** Mtu yeyote au Kiongozi wa Jumuiya atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atapewa adhabu kama ilivyowekwa kwenye Kanuni.

Kanuni ndogo.

**41.**-(1) Baraza linaweza, kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na kwa kuidhinishwa na azimio la wanachama, kutunga Kanuni ndogo ambazo zitafuatwa na wanachama wote wa Jumuiya zinazoelezea jambo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) ada ya mwaka;

(b) sababu na utaratibu unaohusiana na usimamishwaji au ufukuzwaji wa wanachama wa Jumuiya;

(c) udhibiti wa mamlaka yanayotekelezwa na Baraza na kamati yoyote au kamati ndogo ya Baraza na ukasimishaji wa mamlaka;

(d) utaratibu wa kuitisha mikutano ya Baraza, kamati za Baraza, akidi na utaratibu wa uendeshaji wa mikutano ya Baraza;

(e) utaratibu wa uitishaji wa Mkutano Mkuu wa Jumuiya, akidi na utaratibu wa uendeshaji wa Mikutano Mikuu;

(f) utaratibu wa uchaguzi, sifa, uondoshaji na uwekaji wa Rais wa Jumuiya, Makamu wa Rais na wajumbe wengine wa Baraza na wawakilishi wa Jumuiya katika Kamati ya Maadili;

(g) utaratibu wa uteuzi, uondoshaji na uwekaji wa mtu aliyependekezwa na Jumuiya kwenye chombo chochote cha kikatiba au kisheria;

(h) utambuzi, usimamizi na hadhi ya uwanachama wa wanachama wasiokuwa hai;

(i) uhifadhi na matumizi ya muhuri;

(j) njia mbadala za utatuzi wa migogoro zinazojumuisha maridhiano, usuluhishi na upatanishi;

(k) mila na maadili ya taaluma ya wanachama; na usimamizi wa shughuli za kibiashara na matangazo yanayotolewa na wanachama kuhusu huduma zao;

(l) makubaliano ya vigezo na jumuiya nyengine za wanasheria; na

(m) mambo mengine yoyote yanayoweza kuwa muhimu kwa ajili ya kutekeleza malengo na kusimamia masuala ya Jumuiya.

(2) Kanuni ndogo zitakazotungwa na Baraza chini ya masharti ya kifungu hiki, zitawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Jumuiya utakaoitishwa kwa madhumuni hayo.

(3) Kanuni ndogo zitakazotungwa na Baraza chini ya Sheria hii, kabla ya kuanza kutumika zitatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na Mwanasheria Mkuu.

Kanuni.

**42.** Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Kufutwa kwa Usajili na Kubakiza.

**43.**-(1) Msajili wa Jumuiya, mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, atafuta usajili wa Jumuiya ya Mawakili Zanzibar uliofanywa chini ya Sheria ya Jumuiya, Nam. 6 ya 1995.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, majukumu yote, wajibu, mali na madeni ya Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar yaliyokuwepo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, yatahamishiwa moja kwa moja katika Jumuiya iliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 20 Septemba, 2019.

.....................................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***